



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS



TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

MKOA WA KILIMANJARO

Simu : 27- 29 74369

Fax : 27- 29 74368

Email: ded@haidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
S.L.P. 27,
HAI.

Tarehe : 09/08/2021

TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Wilaya ya Hai inatangaza zabuni ya kukodisha magari kwa ajili ya kazi maalumu itakayofanyika tarehe 08/09/2021 hadi tarehe 09/09/2021 ndani ya mipaka ya Halmashauri. Magari yanayohitajika yanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

1. Liwe na uwezo wa kubeba abiria 8, 20, 25, 35 au 40.
2. Liwe na dereva mwenye leseni yenye hadhi ya kuendesha magari ya abiria
3. Liwe na Bima hai (Valid Insurance Cover)
4. Kwa gari lenye uwezo wa Kubeba abiria 8 ni lazima liwe na 4WD
5. Aina ya magari ni Toyota L/Cruiser, Toyota Hiace, Noah na Coaster n.k.

ZABUNI HII INATANGAZWA CHINI YA MASHARTI YAFUATAYO:-

1. Kwa mwombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kuhakikisha gari linafika yadi ya Halmashauri saa 01.00 asubuhi ya tarehe 07/09/2021.
2. Mwombaji atakayeshinda zabuni awe tayari kupeleka gari lake sehemu yoyote atakayopangiwa ndani ya Wilaya ya Hai.
3. Mwombaji ainisha kwenye maombi yake akionyesha aina ya gari, namba ya usajili, bei ya kukodi gari kwa siku moja, uwezo wa gari (idadi ya abiria) na namba ya simu yake kwa ajili ya mawasiliano.
4. Maombi ya zabuni yafungwe kwenye bahasha na kuandikwa juu pembeni zabuni ya kukodi gari na yatumwe kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni(W), S.L.P 27 Hai na zipelekwe ofisi ya ugavi na manunuzi.
5. Mwombaji wa Zabuni atalazimika kumlipa Dereva wake posho ya kujikimu
6. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 16/08/2021 saa 8.00 mchana.
7. Halmashauri ya Wilaya ya Hai hailazimiki kukubali kima cha zabuni cha juu au cha chini.
8. Kazi inayokusudiwa kufanywa na magari haya ni NYETI hivyo ni lazima mwombaji ajiridhishe kuwa gari lake liko katika hali nzuri ya kumudu kazi hiyo bila kuharibika.
9. Gari liwe na ubora na safi.

Herick Marisham

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W).
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI.

MKURUGENZI MTENDAJI (W).
HAI